Toleo La 7: Disemba 2019

# Watu Mazingira

## Ulimwenguni!



**UTAMADUNI DAY**
Uzinduzi wa Washindi wa Tuzo za Watu Mazingira 2019

**Mama Ziro, Mshindi, Tuzo la Mwanamazingira wa Mwaka**

# Yaliyomo


03 **UJUMBE WA KAMATI KUU**

Muktasari wa shughuli na mafanikio ya robo ya 4, 2019 na mtazamo wa mwaka mzima kwa jumla.

04 **TUZO ZA WATU MAZINGIRA 2019**

Juhudi za wanachama 43 katika kuhifadhi mazingira zatambuliwa katika vitengo 7 za Tuzo za 2019.

07 **JUHUDI ZA KUONGEZA MAJI YA KUDUMU KWA KILIMO AFRIKA**

Bw. **Cesario Cambaza** atuarifu kuhusu utafiti wao wa maji na jinsi ya kuboresha kupatikana kwake kwa kilimo.

10 **UKUZAJI WA SOKO LA KOROSHO AFRIKA**

Bw. **John Safari** atoa tarifa ya mikakati ya kuhakikisha Afrika inabaki kuongoza katika uzalishaji korosho ulimwenguni.

12 **MSAFARA MKUU WA KONGONI**

Msafara wa kongoni ni tukio kubwa la 8 la ajabu duniani. Bw. **James Dorop**, kutoka Maasai Mara, Kenya, atupasha zaidi.

15 **ADHABU ZA USIMAMIZI MBAYA WA MAZINGIRA**

Bi. **Hellen Njeri** atujulisha jinsi msururu wa mikasa inapelekea kuundwa kwa sheri za kimazingira Kenya.




**Picha hii ya Kigogota wa Kinubi ilipigwa na Joseph Titus Kangor, P4N-057, katika bonde la Ziwa la Baringo, nchini Kenya.**

# Taarifa ya Kamati Kuu

Kwa mwaka wa pili mfululizo, tumeweza kutoa nakala ya Jarida la Watu Mazingira. Wahariri, wakisaidiana na Ofisi ya Katibu, wamehakikisha tunapata nakala zetu kwa wakati mzuri. Toleo hili ni la 7.

Mtandao wetu wa Watu Mazingira Ulimwenguni, vile vile, umeendelea kukua. Katika mwaka wa 2019, mtandao wetu umeongezeka kwa wanachama 134 zaidi. Wanachama hawa wapya wametoka Bangladeshi (1), Cameroon (2), Ghana (1), Kenya (115), Tanzania (5), Afrika Kusini (1), Uganda (1), Marekani (5), na Zimbabwe (2). Kati ya hao, 32 walikuwa ni vijana chini ya miaka 18 kutoka Bangladeshi (1), Kenya (22), Tanzania (3), Marekani (4), na Zimbabwe (2). Kwa sasa wanachama wetu wamefika 600.

Ofisi ya Katibu iliweza kubuni njia mpya ya kuandikisha wanachama kwa kuzingatia ikoljia wanakotoka. Sasa, wanachama wanaweza kujiandikisha kama kikundi kulingana na mfumo wa ikolojia wanayo ishi, na kuleta pamoja juhudi zao za kukabiliana na changamaoto za ikolojia yao na chumo riziki zao.

Kikundi cha kwanza kuandikishwa kufuatia mfumo huu ni kile cha Wanawake Wanabiashara wa Oloinyototo. Kikundi hiki kilibuniwa Octoba 2019 ili kusadia wanawake kujitosa katika ulingo wa biashara za kimazingira. Kikundi hiki kina mipango ya kuanzisha biashara za ufugaji nyuki, kutengeneza sabuni, kufuga mbuzi wa kisasa na biashara nyingine zenye faida.

Vikundi hivi tunavyoa unda vitasaidia sana kuongeza ushirikiano kati ya wanachama wetu. Ni matumaini yetu pia kuwa vikundi hivi vitaongeza juhudi zetu na kuleta mabadilko yafaayo kwa ikolojia na chumo riziki. Tunawaomba wanachama watuunge mkono na kusaidia katika kukuza vikundi hivi.

Mwaka huu tumeweza kuanzisha vyeti vya uanachama, badala ya kadi za plastiki tulizo anzisha hapo mbeleni. Wanachama wapya na wale wa zamani sasa watapata vyeti hivi, ambavyo vitakuwa na habari zaidi kushinda kadi za zamani. Namba ya mwanachama na siku ya kusajiliwa ni baadhi ya habari mpya ambazo zimeongezwa katika cheti hiki.

Kwa kuhitimisha, kama ilivyo ada ya kufunga mwaka, Tuzo za Mwaka zimeendelea kupa wanachama wetu motisha, kwa kutambua juhudi zao za kulinda na kuhifadhi mazingira. Mwaka huu, wanachama 43 waliweza kutambuliwa katika vitengo 7 (Soma kurasa **4**, **5** na **6** kwa habari zaidi). Katika kitengo cha Tuzo la Familia, tumeweza kupanua na kutambua mzazi mmoja ambaye aliweza kuandikisha watoto wake wote, sio tu kwa 2019, bali kuanzia mwaka wa 2012.

Tuzo za mwaka huu zitakuwa na zawadi mbali mbali kutegemea kitengo cha tuzo, lakini kwa ujumla kutakuwa na cheti na zawadi moja zaidi ya ukumbusho. Kwa shughuli hii, tungependa kutambua Kampuni ya Farm Action kwa mchango wao.

Tunamatumaini kuwa mwaka wa 2020 utakuwa na ufanisi zaidi!

# Tuzo za Watu Mazingira Ulimwenguni 2019

Ni wakati mwingine ambapo tunatambua juhudi za wanachama wetu katika kulinda na kuhifadhi mazingira yetu, na pia kukuza mtandao wetu. Mwaka huu wa 2019, tumevunja ada yetu ya kutangaza washindi Februari na kuwatangaza washindi tarehe 26 Disemba 2019, siku ya kimataifa ya kufungua zawadi za Krisimasi.

Siku hii pia imechaguliwa na Serikali ya Jamhuri ya Kenya kusherehekewa kama Siku ya Utamaduni. Ni kwa sababu hizi, sisi pia tulichagua siku hii kuwatangazia washindi katika vitengo mbalimbali wa Tuzo za 2019.

Wafuatao ni washindi wa Tuzo za 2019 katika vitengo mbalimbali: -

**1. Tuzo la Mwana Mazingira wa Mwaka**

Mama Constance Ziro Kazungu ni mama, mkulima, mwana harakati wa maendeleo ya wakina mama mashinani na mhifadhi mazingira.

Juhudi za Mama Ziro za kulinda na kuacha sehemu za msitu zilizo haribiwa katika shamba lake kukua upya, zimechangia kukua kwa msitu wa ekari 20, katika Kata ya Mwanamwinga, Kaunti ya Kilifi, Kenya. Msitu huu ni moja wa misitu iliyo tumika jadi kama makazi ya jamii asili ya wa Mijikenda, wanao patikana kanda ya pwani ya Kenya. Amekuwa pia mstari wa mbele kuhamasisha wakaazi mashinani kuhusu umuhimu wa kuhifadhi misitu na kuhamasisha wanachama wetu kwa kuchangia taarifa za Jarida letu.

Kwa juhudi zake, alipewa Tuzo la Mwana Mazingira wa Mwaka 2019.


Mbali na kutetea misitu, Mama Ziro amekuwa mstari wa mbele katika kutetea maendeleo ya kina mama na wasichana mashinani, kupitia shirika la Maendeleo ya Wanawake nchini Kenya. Amehudumu kwa muda mrefu kama Mweka Hazina wa shirika hilo, tawi la Kaunti ya Kilifi. Aliweza pia kujitosa katika ulingo wa siasa na kuhudu kama Diwani Maalum, Kaunti ya Kilifi, kuanzia mwaka wa 1997 hadi 2002.



**Mama Constance Ziro Kazungu, Mwana Mazingira wa Mwaka 2019.**

## 2. Tuzo la Balozi wa Mazingira

Tuzo hili limepewa wanachama ambao walisaidia pa kubwa katika kuandikisha wanachama, kukuza ama kusambaza habari muhimu za uhifadhi na habari kuhusu mtandao wetu, kwa wanachama wetu na umma kwa jumla. Wafuatao ndio washindi: -



1. Ahmed Abubakar (Kaunti ya Kwale, Kenya),
2. Amos Sowene (Kaunti ya Taita Taveta, Kenya),
3. Cesario Cambaza (Maputo, Msumbiji),
4. Constance Ziro Kazungu (Kaunti ya Kilifi, Kenya),
5. Halinishi Yusuf (Kaunti ya Makueni, Kenya),
6. Hezekiah Karanja (Kaunti ya Nyandarua, Kenya),
7. Janet Mueni Matheka (Kaunti ya Mombasa, Kenya),
8. James Dorop (Kaunti ya Narok, Kenya),
9. John Safari, aliye pigwa picha hapo juu, (Kaunti ya Kilifi, Kenya), aliweza kuandika taarifa nyingi zaidi katika jarida letu mwaka wa 2019,
10. Kariuki Wachira (Kaunti ya Nyandarua, Kenya),
11. Kusundwa Wamalwa Kusundwa (Katavi, Tanzania),
12. Omar Juma Abdallah (Kaunti ya Kwale, Kenya),
13. Paige Samblanet (California, Marekani),
14. Paul Omonge (Kaunti ya Nakuru, Kenya),
15. Ruth Kagai Adeka (Kaunti ya Nairobi, Kenya),
16. Hellen Njeri Kuria (Kaunti ya Kilifi, Kenya).

## 3. Tuzo la Hazina Mazingira

Walio tuzwa ni wanachama walio weza kuchangia akaunti zao za Hazina Mazingira bila kulegea, kuchukua na kulipa mikopo kwa wakati unao faa, ama kuwahamasisha wengine kuweza kujiunga na kutumia Hazina Mazingira.

1. Noombarbali Enole Soit, Kaunti ya Narok, Kenya kwa kuweza kuhamasisha jamii yake na kuwasaidia kufungua akaunti na Hazina Mazingira,
2. Karen Magomere Shavola, Kaunti ya Kakamega, Kenya, kwa kuwa na shughuli nyingi za kuweka na kutoa katika akaunti yake ya Hazina Mazingira,
3. Mariam Hamisi, Kaunti ya Taita Taveta, Kenya, kwa kuweza kulipa mkopo kwa wakati unao faa.

## 4. Tuzo la Kazi ya Pamoja

Viongozi wa Kikundi cha Oloinyototo waliweza kuonyeza kazi nzuri ya kikoa iliyo wawezesha kuhamasisha wanawake katika Kijiji cha Olesere eneo la Maasai Mara kuanzisha Kioto cha Biashara cha Wanawake wa Oloinyototo.

Viongozi hawa ni Noombarbali Enole Soit, Evelyne Dorop, Faith Resian Morompi na Noonkuta Enole Dorop kutoka Kaunti ya Narok, Kenya.

## 5. Mfanyikazi Bora wa Mwaka

Tuzo hili liliwaendea **James Kapoto Dorop** na **Sally Titoyia Sengeny** (walio pigwa picha hapa chini), wote wawili kutoka Kaunti ya Narok, Kenya.



## 6. Tuzo la Vijana

Tuzo hili lilitambua juhudi za kuonekana za vijana chini ya miaka 18 katika uhifadhi wa mazingira. Washindi wa mwaka huu ni wasichana wawili,



1. **Salome Ndechikio**, kwa picha, kutoka Kaunti ya Taita Taveta, Kenya, ambaye yuko darasa la 4, kwa upanzi wa miti, na
2. **Naomi Cidi**, kutoka Kaunti ya Kilifi, Kenya, ambaye yuko darasa la 5, kwa juhudi zake kama Skauti wa Kike na usimamizi wa shamba dogo la mboga.

## 7. Tuzo la Familia

Tuzo hili lilitambua wanachama ambao waliweza kuandikisha familia zao katika mtandao wa Watu Mazingira katika mwaka wa 2019, na wazazi wa pekee walio andikisha familia zao lakini wakakosa zawadi hii katika miaka ya awali kwa sababu ya kukosa kuandikisha mzazi wa pili.

1. **Ashengai Abel Kimath** (Arusha, Tanzania),
2. **Domitila Nzomo** (Kaunti ya Taita Taveta, Kenya),
3. **Dkt. Muktarun Islam Prity,** (Sylhet, Bangladesh),
4. **Esther Wambui Karanja** (Kaunti ya Nyandarua, Kenya),
5. **Grace Njeri Njoroge** (Kaunti ya Nairobi, Kenya),
6. **Halinishi Yusuf** (Kaunti ya Makueni, Kenya),
7. **Hezekiah Karanja** (Kaunti ya Nyandarua, Kenya),
8. **John Safari** (Kaunti ya Kilifi, Kenya),
8. **Karen Shavola** (Kaunti ya Kakamega, Kenya),
9. **Mary Kahonzi** (Kaunti ya Kilifi, Kenya),
10. **Phathisani Tabengwa** (Bulawayo, Zimbabwe),
11. **Rashida Zaid Suleiman** (Arusha, Tanzania),
12. **Samuel Chanzi** (Philadelphia, Marekani). Bw. Chanzi aliandikisha wanachama 5 wa familia yake, na kuwa mwanachama aliye andikisha wanachama wengi zaidi, 2019,
13. **Sheillah Kemunto** (Kaunti ya Nyamira, Kenya),
14. **Tabitha Ndonga** (Kaunti ya Taita Taveta, Kenya).



**Bi. Halinishi Yusuf akita na mwanawe, Che.**



**Bw. Samuel Chanzi akita na familia yake. Wakati huu, Sarah Mulana, mwanachama wa kwanza kusajiliwa 2019, alikuwa hajazaliwa.**

# Juhudi za Kuongeza Maji Ya Kudumu Kwa Kilimo Afrika

Katika mwongo mmoja uliopita, kumekuwa na upungufu wa mazao ya kilimo katika eneo la Sahara, Afrika. Kuna vizuizi vinavyo changia hali hii, kama vile mapungufu ya rotuba, maji, kawi, soko na mbinu zilizo pitwa na wakati za kilimo nyanjani.

Katika sehemu kame, maji kidogo na yasiyo patikana kwa urahisi, imekuwa changamoto kubwa kwa ukuzaji mimea. Ukosefu wa maji ya kudumu umezuia matumizi ya mbolea na kuchangia kuwepo kwa mazao hafifu. Hali hii inakuwa mbaya zaidi katika maeneo yaliyo athiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa, iwapo ni mafuriko ama ukame.

Njia moja ya kuongeza uwezo wa kuberesha mazao ya kilimo katika eneo la Sahara ni kuthibiti uwepo wa maji kwa kuwa na mfumo wa kilimo unao stahimili mabadiliko ya hali ya hewa na kuhifadhi maji, hasa katika udongo. Mfumo mzuri wa kilimo unaweza kuongeza matumizi ya maji hafifu.

Mito ya msimu inaweza kuwa sehemu asili ya kuhifadhi maji. Mchanga katika vitanda vya mto vina uwezo wa huhifadhi kiasi kizuri cha maji msimu mzima wa ukame, na kuweza kutumika kunyunyizia mashamba. Kuna utafiti unao endelea wa kutafuta suluhu ya kuhakikisha maji haya yanaweza kutumika kikamilifu na jamii ili kuongeza kilimo biashara.

Mradi huu wa utafiti unanuia kuboresha njia zilizotumika tangu jadi za maji yanayosama kwa mchanga na kufanya njia hizi kuwa bora na endelevu kutumia 'maabara hai' ili: -

1. Kusaidia wakulima kutumia mifumo mipya ya kilimo ili kuboresha chumo riziki,
2. Kuongeza ubunifu unao weza kubadilisha desturi za wakulima na kuwahimiza kutumia njia bora zaidi na kushirikiana zaidi,
3. Kukuza ushirikiano na kujifunza baina ya nchi zinazoendelea na baina ya nchi zinazoendelea na nchi zilizoendelea, na kuboresha utafiti.

Wanao tekeleza mradi huu ni mashirika ya IHE Delft (kiongozi), Chuo Kikuu cha Makelle, Oxfam Msumbiji, Dabane Trust, ACACIA Water na Oxfam Novib. Washiriki walio katika maabara ya Limpopo ni Oxfam Msumbiji (mshirikishi), Chuo cha Juu cha Kiufundi cha Gaza, Chuo Kikuu cha Eduardo Mondlane, ARA-Sul, Taasisi ya Kitaifa ya Unyunyiziaji Maji, Shirika la Maendeleo ya Jamii Mashinani, iDE ma Kulima. Mradi huu unatekelezwa kwa miaka 3 kuanzia 2016 hadi 2019, na kupata kuongezwa muda hadi Septemba 2020.



**Bw. Cesario Cambaza (pichani), na Bw. Paulo Saveca, waandishi wa taarifa hii, ni wahadhiri na watafiti wa Chuo cha Juu cha Kiufundi cha Gaza, nchini Msumbiji.**

### Utafiti Eneo la Limpopo (Msumbiji)

Sehemu kame mara nyingi huwa na mito yenye mchanga mwingi (picha 1), na huonekana punde tu kunapo nyesha. Mchanga unao patikana katika mito hii husaidia kuhifadhi maji, ambayo huongezeka kila mara kunapo nyesha.



**Picha 1: Bonde la mto wenye mchanga mwingi. Mto huu unaonekana punde tu kunapo nyesha.**

Mradi huu uliweza kuchapisha ripoti ya uchunguzi wa uwezekano wa kufaulu kwa mradi mwezi wa Machi 2019. Hii ni baada ya utafiti uliofanywa kuanzia Janauri hadi Disemba 2018, uliolenga unyunyiziaji kutumia maji yaliyo hifadhiwa kwa mchanga katika bonde za mito. Uchunguzi huu uliangalia uwezekano wa kitaalam, kufaulu kwa biashara za kilimo na uwezo wa matokeo ya utafiti kuweza kutumika katika eneo la mto Limpopo nchini Msumbiji.

Uchunguzi huu ulifanywa na wataalam kutoka ACACIA Water (kiongozi), Chuo cha Juu cha Kiufundi cha Gaza, Oxfam Msumbiji, Shirika la PRACTICA na IHE Delft, wakisaidiwa na Serikali ya Msumbiji na kufadhiliwa na Serikali ya Uholanzi.

Kuna njia tofauti zilizotumika katika utafiti wa 2018, ikiwemo uchimbaji kwa mkono (picha 2 na 3), kutengeneza kisima kutumia vifaa vinavyo patikana mashinani na pia ufanya kazi wa bomba za unyunyiziaji maji kutumia kawi ya jua. Matokea ya utafiti huu




**Picha 2: Mbinu ya kuchimba kisima.**

ulionyesha kuwa maji hupatikana mita 3 hadi 5 katika mchanga wa bonde la mto mkavu. Mchanga katika sehemu hii ulionekana kupangika safu moja juu ya nyingine hadi kina cha mita 13.6. Utafiti pia ulibaini kuwa sehemu hii ina uwezo wa kutoa maji mchemraba 18 kwa saa (18m3/saa) kutoka mita 3.84 kwa wastani. Kina hiki hupungua wakati wa mvua na kuongezeka wakati wa ukame. Maji yalipatikana kuwa yafaa kwa unyunyiziaji mashamba kwa kuto kuwa na chumvi.



**Picha 3: Mbinu ya kuchimba kisima.**

Zaidi ya haya, kuna mashamba ya majaribio ambayo yalitayarishwa kwa unyunyiziaji kutumia bomba za kunyunyizia maji kutumia kawi ya jua (picha 4). Bomba hizi ziliwekwa katika mashamba manne katika wilaya ya Chókwè na Guijà, mkoa wa Gaza. Mabomba haya yalichaguliwa kuweza kufikia mahitaji ya kila mkulima kwa kuangalia aina ya bomba, mpangilio wa kufikisha maji shambani na matumizi ya maji shambani.



**Picha 4: Picha inayo onyesha maji yaliyo hifadhiwa mchangani na mfumo wa kusambaza maji ya unyunyiziaji mashamba.**

Ubunifu huu umeletea wakulima wadogo manufaa kwa njia tatu: ufundi uliotumika (uchimbaji wa visima kwa mkono karibu na bonde la mto, pamoja na bomba la kunyunyizia maji kutumia kawi ya jua), mpangilio (mkulima binafsi), na madhumuni (kilimo biashara). Utafiti huu ulionyesha kuwa gharama ya kunyunyizia shamba la mita 2,000 mraba ni kati ya dola za Marekani 675 na 1,420. Kwa wakati huu, mkulima mdogo anapata faida ya dola 750 kwa hekta kwa msimu mmoja, ambayo inaweza kulipa gharama yote ndani ya miaka 3. Utafiti pia ulibaini kuwa mpangilio huu unaweza faa kwa shamba la hekta 47,400, inayonyunyiziwa maji kiasi cha 150mm3 kwa mwaka.

Mradi unaruhusu mkulima kutoa maji kutoka kwa mto mkavu na kutumia kwa unyunyiziaji shamba. Mwaka wa 2019, Bi. Anita (Picha 5), mwenye miaka 65 kutoka eneo la Macarretane, wilaya ya Chókwè, alipata vifaa hivi na kutumia kwa misimu miwili mfululizo. Bi Anita awali alikuwa akitegemea mvua kwa kilimo na kukuza mahindi tu. Kwa kutumia vifaa hivi, ameweza kulima shamba mita 2,000 mraba na kupanda mimea tofauti tofauti, ikiwemo mahindi, kabichi, na maharagwe. Mazao haya aliweza kuyauza sokoni na kupata faida ya dola za Marekani 83,000, na kuongeza mapato yake nyumbani. Mapato haya yamemuezesha kununua mbegu kwa msimu mpya bila usaidizi. Kwa sasa Bi. Anita ana maji wakati wote wa mwaka, kwa gharama ndogo kwa kutumia bomba la maji la kutumia kawi ya jua.

Kwa kuhitimisha, utafiti huu umeonyesha kuwa wakulima 30,000 katika eneo la chini la Limpopo wanaweza kunyunyizia angalau hekta 15,000 kwa mimea shambani. Kwa hivyo, vifaa hivi vinasaidia kuongeza maji ya kudumu kwa ukulima, kuwezesha kilimo biashara na kuongeza faida ya mkulima. Ili wakulima wengi waweze kufaidika na vifaa hivi, kuna umuhimu wa Serikali au wafadhili kuunda mbinu za wakulima kupata mikopo rahisi, na hasa kutoka kwa mashika yenye uzoefu wa kutoa mikopo ya kilimo. Kwa kuongezea, mradi huu una uwezo wa kuzalisha chakula cha kudumu na kuongeza mapato kwa mamia ya wakulima wanaotegemewa na familia zao nchini Msumbiji.





**Picha 5: Bi. Anita (pichani juu), akiunganisha bomba la kunyunyizia maji shambani kwa paneli ya kawi ya jua, na (pichani chini), baada ya kuvuna kabichi kutoka shambani kwake.**

# Ukuzaji Wa Soko La Korosho Afrika



Bara la Afrika lime changia pa kubwa katika ukuzaji wa kilimo wa zao la korosho. Katika mwaka wa 2015, wakulima milioni 2.5 wadogo wadogo wa Afrika waliweza kuzalisha asli mia 57 ya zao la korosho ulimwenguni. Kati ya waka wa 2006 na 2015, uzalishaji wa korosho ulikuwa kutoka tani 35,000 hadi tani 105,700.

**Umuhimu wa Kilimo cha Korosho kwa Bara Afrika**

Thuluthi mbili za wakazi wa Afrika hutegemea kilimo kwa chumo riziki. Lakini changamoto kubwa inayo kumba nchi za Afrika leo hii ni jinsi ya kufanya kilimo kuwa endelevu na kuweza kukimu mahitaji ya sasa na ya siku zijazo.

Umuhimu na umaarufu wa mkorosho umeanza kuongezeka katika nchi nyingi na kuonekana kama zao muhimu la biashara lenye uwezo mkubwa. Na kwa vile athari za mabadiliko ya hali ya hewa yameanza kuonekana na kulazimisha wakulima wengi, hasa wa eneo la Sahel, kutafuta mbinu mbadala, zao la korosho linaonekana la faa katika mazingira haya ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Mazao mengi ya biashara Afrika yana kumbana na changamoto nyingi katika kukabiliana na hali mbaya ya hewa. Ni kwa sababu hii zao la korosho linatoa nafasi nzuri kwa wakulima wadogo kubuni njia mbadala ya kuunda mfumo bora wa kilimo cha siku za usoni. Korosho pia inatoa nafasi nzuri ya kuongeza uzalishaji na kupanua nafasi za kazi. Kuongezea, korosho ikiuzwa nje ya nchi inasaidia kupanua soko la kimataifa.

**Changamoto**

Sekta ya korosho bado ni changa na yenye changamoto nyingi. Wakulima wadogo na wenye viwanda bado hawajajipanga vizuri. Kwa mfano, kuna upungufu wa mashirika ya wakulima, ukosefu wa mashirika yanayotoa mikopo kwa wakulima na ujuzi wa kusimamia sekta nzima kwa ujumla. Kwa kuongezea, nchi nyingi hazitoi usaidizi wa kutosha, kama vile kanuni bora na miradi ya kukuza sekta ya korosho.

**Kukuza Sekta ya Korosho**

Serikali nyingi Afrika zimeanza kutambua umuhimu na uwezo wa sekta ya korosho. Ni kwa sababu hii, Baraza la Mashauri ya Kimataifa la Korosho lilibuniwa nchini Ivory Coast mwaka wa 2016. Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa shirika la kimataifa la zao la kilimo kuundwa kutokana na juhudi za nchi za Afrika. Lengo kuu la shirika hili ni kuunda na kukuza sekta ya korosho kupitia ubadilishanaji wa habari.

Mnamo tarehe 17 Novemba 2016, nchi nne za Benin, Ivory Coast, Togo na Burkina Faso, walitia sahahi makubaliano ya kunzisha shirika hili. Kufikia sasa, shirika hli lina wanachama tisa, Benin, Burkina Faso, Ivory Coast, Ghana, Guinea, Guinea-Bissau, Mali, Togo and Senegal, na kwa pamoja, wanawakilisha asili mia 42 ya nchi zote ulimwenguni zinazo kuza zao hili.

Shirika la Ubora wa Korosho ni kioto kingine kilicho buniwa na nchi za Afrika kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa koroho na kupunguza umaskini kati ya wakulima wadogo katika nchi sita zilizo anzisha mradi huu. Nchi hizi ni Benin, Burkina Faso, Ivory Coast, Ghana, Msumbiji na Sierra Leone.

Shirika la Ubora wa Korosho linatoa nafasi ya muundo mpya wa kuleta wadau wengi katika ushirikiano wa kukuza uzalishaji na uboreshaji wa zao la korosho. Shirika hili ni mradi unaoleta pamoja washika dau kutoka sekta ya umma na ya kibinafsi, chini ya shirika la kiJerumani la Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ), na kufadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Maendeleo ya Kiuchumi ya Ujerumani.

Kwa ushirikiano na makampuni ya kibinafsi na mashirika ya umma, hatua kubwa zimepigwa na ufanisi mkubwa kupatikana kwa wakulima zaidi ya 512,000 na kampuni za viwanda 40. Tangu mradi huu uanzishwe, nafasi 530,000 za kazi zimebuniwa katika nchi za Benin, Burkina Faso, Ivory Coast, Ghana, Mozambique na Sierra Leone – asili mia 75 katika uzalishaji, asili mia 20 katika biashara na asili mia 5 katika viwanda.

Shirika la Ubora wa Korosho lilianzishwa 2009 na kwa sasa liko katika awamu ya tatu ya utekelezaji, ambayo itaisha Disemba 2020.

Kuna malengo makubwa manne ya mradi huu katika awamu hii ya tatu ya utekelezaji: -

1. Kuongeza uzalishaji wa korosho kwa wakulima,
2. Kujenga uwezo wa viwanda mashinani kufikia kiwango cha kimataifa,
3. Kujenga uhusuano bora na thabiti wa kibiashara kati ya wazalishaji, makampuni ya viwanda na wanunuzi,
4. Kutengeneza mazingira mazuri ya sekta kama vile utengenezaji wa kanuni bora za kusaidia kukuza sekta ya korosho.

Katika awamu hii ya tatu, mradi huu una lenga kuleta pamoja mafanikio ya awali ya mradi huu, kuongeza uwezo wa wadau mashinani, na kuelimisha washirika. Kufuatia mpangilio huu, mradi umeongeza juhudi za kujenga uwezo wadau kupitia Mpango Mkuu wa Mafunzo. Mpango Mkuu wa Mafunzo una lenga kikosi cha wataalam watakao saidia kuelimisha na kubuni njia mpya za uzalishaji na kuboresha zao hili hadi kufika sokoni.

Kupitia kwa mpango wa mafunzo, kuna wataalam katika kila nchi kusaidia na kusambaza elimu ya: -

1. Usimamizi wa mashamba ya korosho,
2. Usimamizi wa ubora wa korosho baada ya kuvuna,
3. Uongezaji thamani wa zao la korosho,
4. Uboreshaji wa soko la korosho,
5. Uhusiano wa kibiashara kati ya wadau,
6. Mipango ya kuongeza ubora bidhaa ya korosho,
7. Uchumi wa uzalishaji wa korosho,
8. Ushauri wa kujitaftia fedha za kuongeza mazao na soko la korosho,
9. Changanuzi na utengenezaji wa bei, na
10. Utengenezaji wa vifaa vya mafunzo.

Kufikia sasa, wataalam 291 wamepata mafunzo haya, na kati yao 78 ni wanawake.

.



**Bw. John Safari Ziro (mstari wa mbele kulia), mwandishi wa taarifa hii, akihudhuria Mpango Mkuu wa Mafundisho katika mji wa Sunyani, nchini Ghana, kuanzia tarehe 24 Agosti hadi Septemba 1, 2019. Mashiriki 98 walihudhuria mafunzo haya, wakiwakilisha nchi za Benin, Burkina Faso, Ivory Coast, Ghana, Kenya, Mozambique na Sierra Leone.**

# Msafara Mkuu wa Kongoni



Msafara wa kuhama kwa mamilioni ya punda milia, kongoni na wanyama wengine katika eneo la Africa Mashariki ni kivitio kikubwa cha wapenda safari za mbuga.

Na kwa wapenda safari za mbugani, ni muhimu kupata habari kamilifu za uhamiaji huu ili waweze kupanga maeneo ya kukita kambi na maeneo mazuri la kuona maajabu haya ya ulimwengu.

Kila mwaka, takriban kongoni milioni 2 na wanyama wengine wa mbugani elfu 20 huhama kutoka Serengeti nchini Tanzania hadi Maasai Mara, kusini mwa Kenya, kutafuta malisho mazuri na maji.
I
Msafara huu, wenye hatari nyingi, huelekea maeneo ambayo kuna nyesha. Mzunguko wote wa msafara huu usio isha ni karibu kilomita 3000.
Msafara huu ni kivutio kikubwa kwa wapenda safari za mbuga, wapenda mazingira na watalii wanao penda kuona mapya Afrika.

**Msafara wa Uhamiaji**

Takriban kongoni milioni 2 na wanyama laki 3 wakiwemo punda milia, hukusanyika katika mbuga za Serengeti na kuanza msafara kuelekea kaskazini hadi Mbuga ya Kitaifa ya Maasai Mara, nchini Kenya.

Msafara huu ni wa kutafuta lishe na maji. Msafara hufuata mzunguko wa akrabu na wanyama hukamilisha karibu kilomita 3000. Safari huwa na changamoto nyingi na kila mwaka angalau kongoni 250,000 hufa njiani.

Moja ya vivutio vikubwa vya msafara huu ni wakati wanyama wanapo kusanyika kuvuka mto Grumeti. Hapa mamba husubiri wale wanyama wanyonge wasio weza mawimbi ama kupoteza mama zao, na kuwafanya kitoweo.

Mbali na vnivukio hivi, kuna vivutio vingine pia. Kuona umati mkubwa wa wanyama hawa wakiwa mbugani ni jambo la kuvutia mno. Umati huu wa wanyama huvutia wanyama wengine kama vile simba, chui, fisi na mbwa mwitu, na kupatia watalii fursa ya kuona wanyama hawa wakiwinda.

**Kwa vile tukio hili ni la kiasili, kuhama kwa wanyama hawa hubadilika mwaka baada ya mwingine kulingana na majira na eneo.**



## Msafara Nchini Tanzania

Kuanzia Disemba hadi Machi, mbuga za Serengeti na Maeneo ya Uhifadhi ya Ngorongoro kaskazini mwa Tanzania, hujaa kundi kubwa la kongoni, punda milia na wanyama wengine. Wakati huu pia ni msimu wa wanyama hawa kuzaa.

Kongoni wengi huzaa katika kipindi cha wiki tatu, hasa mwanzoni mwa Februari. Kuzaliwa kwa ndama wengi na kuwaona wakikimbia karibu na mama zao huvutia sana. Ndama pia huvutia wanyama wawindaji, na wakati huu wa mwaka, ni wakati mzuri wa kuwaona wakiwinda.

Watalii wanaopenda kuona msafara huu, wana fursa nzuri ya kuwaona kusini mwa Ndutu na mbuga za Salei.

Kuanzia Aprili hadi Mei, msafara huanza kuelekea maghniaribi na kwenye malisho bora na mwitu ulio ushoroba ya Serengeti magharibi. Huu ni msimu wa mvua na ni vigumu kufuata msafara wa kongoni, hasa kwa vile barabara nyingi hazipitiki na kambi nyingi huwa zimefungwa.

Kufikia mwisho wa Mei, mvua zinaisha. Kongoni na punda milia hukusanyika tena na kuanza safari kuelekea kaskazini. Wakati huu kongoni hupandisha. Kwa watalii, magharibi mwa Serengeti ni eneo bora la kuona msafara huu.

Msafara hufika mto Grumeti Julai na kukumbana na changamoto kubwa ya kwanza. Mto Grumeti huwa na kina katika sehemu nyingi, hasa kama kumenyesha vizuri. Hapa watalli wana fursa ya kuona umati mkubwa wa wanyama wakivuka. Kwa vile mto una kina, kuna uwezekeno wa kuona wanyama wakizama na kuliwa na mamba.

## Msafara Nchini Kenya

Nyasi magharibi mwa Serengeti hubadilika kahawia mwishoni mwa Julai na msafara unaendelea na safari ya kaskazini. Baada ya kuvuka mto Grumeti, nchini Tanzania, kongoni na punda milia huingia chembeo cha Lamai na eneo la Mara Triangle.

Kabla kuingia maeneo ya Mara yenye nyasi nyingi, msafara wa wanyama lazima wavuke mto Mara. Mto Mara huwa pia umejaa mamba.

Kongoni, punda milia na wanyama wengine hujaza mbuga za Mara, kuanzia Septemba hadi Novemba, wakiandamwa na wanyama wawindaji.

- Uzio wa singenge umekuwa maarufu maeneo ya Mara-Loita. Kugawanyika kwa vikundi vinavyo simamia mashamba ya jamii umepelekea watu binafsi kuweka uzio kwa mashamba yao.
- Ongezeko la watu na mifugo ndio tisho kubwa zaidi. Kuna mabadiliko ya matumizi ya mashamba kutoka kwa ufugaji hadi ukulima na ongezeko la mitafaruku baina ya binadamu na wanyama pori,



**Kongoni wakivuka mto Mara uliojaa mamba nchini Kenya.**

Mvua za Novemba na Disemba huanza majira haya upande wa Tanzania, na wanyama huanza safari yao ya kurudi mbuga za Serengeti. Wakirudi Serengeti, kongoni kuzaa.

## Tisho Kubwa kwa Kongoni

- Vitisho vinavyo kumba kongoni ni tofauti kulingana na maeneo wanako pitia,
- Sababu kuu zinazopelekea kupungua kwa kongoni ni mipango duni ya upanuzi wa kilimo, ua za singenge, makazi, chipuko la miji, barabara na miundo misingi, uwindaji haramu, mifugo wanao pia tegemea mbuga kwa malisho na maji,
- Ukosefu wa utekelezaji wa sera kumepelekea kuwepo kwa makazi maeneo yasiyo faa,
- Udhaifu mkubwa wa Serikali ya Kenya ni kupa kupao mbele mbuga zilizo chini ya usimamizi wa Serikali. Mbuga hizi zinachukua eneo la asili mia 8 lenye asili mia 35 ya wanyama pori ikilinganishwa na asili mia 65 ya wanyama pori wanaopatikana katika arthi ya watu binafsi. Ni katika arthi hii ya watu binafsi ambako kongoni wako katika hatari kubwa wanapo hama.

## Ukweli Wakupendeza

1. Kongoni hujulikana pia kama gnu kwa sababu ya mlio wa 'gnu gnu gnu' wanao toa,
2. Katika kipindi cha wiki tatu kila mwaka, ndama wa kongoni 400,000 huzaliwa. Wingi wa ndama huhakikisha kuna chakula cha kutosha kwa wanyama wawindaji na hivyo basi wengi wao huepuka kuwindwa,
3. Kongoni wana uwezo wa kukimbia dakika kidogo baada ya kuzaliwa,
4. Hakuna mtafaruku baina ya kongoni na punda milia wakati wa malisho kwa vile kila mmoja hupendelea sehemu tofauti ya nyasi,
5. Hakuna punda milia wawili wanao fanana,
6. Ina kadiriwa kuwa kongoni 250,000 hufa katika msafara huu kila mwaka,
7. Msafara wa kongoni ni tukio lililo anza miaka ya 1960.



**Bw. James Kapoto, muandishi wa makala, anaishi na kufanya kazi eneo la Maasai Mara. Yeye hufanya kazi na Mbuga ya Uhifadhi ya Naboisho, na mara nyingine hupata fursa ya kusaidia na kazi za Shirika la Africa Nature Organization katika eneo hili.**

# ATHARI ZA USIMAMIZI MBAYA WA MAZINGIRA



**Bwawa la Patel Milmet, lililo jengwa kwa kingo za udongo, linamilkiwa na watu binafsi, eneo la Solai, Kaunti ya Nakuru, Bonde la Ufa, Kenya. Kufuatia mvua kubwa iliyonyesha, bwawa lilivunja kingo zake tarehe 9 Mei 2018, na kuua watu 48.**

Habari za kuporomoka kwa jengo la shule ya msingi ya Precious Talent jijini Nairobi tarehe 23 Septemba 2019, ziliwashangaza na kuwa huzunisha wengi, hasa baada ya wanafunzi 8 kuaga dunia. Mkasa huu unafuatia ule wa Solai, Kaunti ya Nakuru, ambapo bwawa la Patel lilivunja kingo zake na kuwaua watu 48. Mbali na maafa haya, kuna maafa zaidi yaliyo sababishwa na hali mbaya ya mazingira. Maafa yanayo tokana na hali mbaya ya mazingira yatazidi kuonekana ikiwa mikakati haita wekwa kuyazuia.

Mikasa inayo tokana na mazingira ina uhusiano na usimamizi duni wa serikali za Kaunti na ya Kitaifa kwa kukosa kutekeleza wajibu wao. Katika ngazi ya kitaifa, Halmashauri ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira imemulikwa kwa kuwa ndio shirika lenye jukumu la kulinda mazingira kwa kuhakikisha sheria na kanuni za mazingira zinafuatwa.

Nchi ya Kenya ina katiba na sheria nzuri ya mazingira – Sheria ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira. Sheria hii imepata nguvu zaidi kutokana na kanuni za Tathmini za Athari ya Miradi kwa Mazingira ya 2003. Sheria hizi za mazingira zinasaidia kuepukana na mikasa, ikiwa zitafuatwa.
Hata baada ya miaka 20 baada ya kupitishwa kwa sheria hizi, kuna uzembe katika kuzitekeleza. Hali hii imefanya utekelezaji wa miradi ya kibinafsi na ya umma kuwa hatari kwa usalama wa mazingira nchini. Kama tuna sheria mwafaka za mazingira, shida iko wapi?

Miradi na shughuli zinazo weza kuathiri mazingira kwa njia moja ama nyengine, lazima zifanyiwe utathmini wa athari zake kwa mazingira kabla kupata kibali cha kuitekeleza. Lakini kuna tetesi na malalamishi mengi kuhusu utekelezaji wa tathmini hizi nchini Kenya. Inaonekana, pia, kuwa kanuni za tathmini za athari za mazingira za 2003 zimepitwa na wakati, hasa matakwa ya uwazi kwa wanaotekeleza miradi inayotegemea mazingira na mali asili. Kwa mfano, sekta ya ujenzi, wachimba migodi na uvunaji wa maji.

Kanuni za Tathmini ya Athari za Miradi kwa Mazingira ya 2003 haziko kamilifi kuweza kukabiliana na chimbuko la athari zinazo letwa na miradi ya maendeleo. Kwa mfano, kanuni hizi hazi angazii waendelezaji binafsi wasio hofu ya kwenda kinyume na kanuni hizi na kutapeli jamii mashinani.

Waendelezaji binafsi wamezoea kutumia hongo kulazimisha matakwa yao bila kujali maslahi na maisha ya wa Kenya. Mara nyingi, kilio cha umma hupuuzwa na Serikali ya Kitaifa na za Kaunti, hadi pale maafa yanapo tokea.

Punde tu maafa yanapo tokea, hutokea shughuli nyingi, ikiwemo kushikwa kwa wahusika. Wiki moja baadaye, shughuli za kawaida zilizo leta maafa haya, huendelea tena, hadi pale maafa mengine yatakapo tokea tena. Inaoneka, hitoria haitufunzi chochote.

Mwaka wa 2018, Halmashauri ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira iliweza kuleta pamoja wizara muhimu, mashirika ya kibinafsi na ya umma, katika mchakato wa kuboresha Kanuni za Tathmini ya Athari za Mazingira za 2003. Mchakato huu ulifaulu kuzindua kanuni kielelezo cha Tathmini Kamilifu na Ukaguzi wa Athari ya Miradi Mikubwa na Midogo kwa Mazingira cha 2018.

Kanuni Kielelezo cha 2018 kiko sambamba na Sheria iliyo fanyiwa marekebisho 2015 ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira, kifungu cha 387 cha Sheria za Kenya. Kanuni mpya zinalenga maswala chipuka kama vile Tathmini Kimkakati ya Mazingira, mipangilio ya kulinda mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa, serikali za ugatuzi, mageuzi ya haraka ya matumizi ya arthi na teknolojia mpya.

Wadau wengi wamekuwa wakisubiri kwa hamu kupitishwa kwa kanuni hizi mpya. Badala yake, wadau wlipigwa na bumbuwazi, mwanzoni mwa 2019, pale Waziri wa Mazingira na Misitu alichapisha Tangazo la Kisheria namba 32, iliyo rekebisha kipengele kimoja tu cha kanuni za 2003. Wadau wengi waliachwa wakijiuliza kama kanuni kielelezo cha Tathmini Kamilifu na Ukaguzi wa Athari ya Miradi Mikubwa na Midogo kwa Mazingira cha 2018 kilitupiliwa mbali.

Kwa kutilia maanani mapungufu ya kanuni za 2003, juhudi kubwa za wadau katika kutengeza kanuni mpya za 2018 ili kurekebisha mapungufu haya, Muungano wa Kitaifa wa Mashirika ya Mazingira, wanamhimiza Waziri achapishe kanuni hizi katika gazeti rasmi la Serikali. Tangazo la Kisheria namaba 32, lina mapungufu mengi na isiyo fuata utaratibu wa sheria inayo jaribu kuibadilisha.

Kuongezea, Tangazo hili linatoa nafasi kwa Serikali ya Kitaifa na ya Kaunti kuendelea kuzembea katika majukumu yao ya kulinda na kuhifadhi mazingira. Kwa mfano, Tangazo hili linatoa ruhusa kwa miradi ya athari za kadri na ile ya athari za chini kuweza kupitishwa bila kufanyiwa tathmini kamilifu.

Kulingana na Tangazo hili, miradi ya athari za kadri na ile ya athari za chini inaweza kupitishwa na maafisa ambao hawajafanya hii kazi vizuri siku zilizopita. Muungano wa Kitaifa wa Mashirika ya Mazingira unapendekeza kuondolewa kwa Tangazo la Kisheria namaba 32, na badala yake kanuni za Tathmini Kamilifu na Ukaguzi wa Athari ya Miradi Mikubwa na Midogo kwa Mazingira ya 2018 ichapishwe katika gazeti rasmi la Serikali.



**Bi Hellen Njeri Kuria, katikati, mwandishi wa makala, akionekana hapa na wanachama wenzake wa Muungano wa Kitaifa wa Mashirika ya Mazingira nchini Kenya, wakati wa warsha ya kupiga msasa makala haya na kuunda mkakati wa utetezi kushindikiza kuchapishwa kwa kanuni kielelezo ya Tathmini Kamilifu na Ukaguzi wa Athari ya Miradi Mikubwa na Midogo kwa Mazingira ya 2018.**

**Makala haya yalichapishwa awali katika shirika la utangazaji la K24, Novemba 14, 2019. (https://www.k24tv.co.ke/opinion/manage-the-environment-or-it-will-fight-back-necsa-kenya-12163/)**

# KARIBUNI NYUMBANI!


Katika mwaka wa 2019, mtandao wa Watu Mazingira uliongezeka kwa wanachama 134. Wanachama hawa walitoka Bangladesh (1), Cameroon (2), Ghana (1), Kenya (115), Tanzania (5), Afrika Kusini (1), Uganda (1), Marekani (5), na Zimbabwe (2). Kati ya hao, 32 walikuwa vijana chini ya miaka 18 kutoka Bangladesh (1), Kenya (22), Tanzania (3), Marekani. (4), na Zimbabwe (2). Tuwakaribisheni NYUMBANI!



**Rifah Nanjiba Sneha, akiwa na mamake Dkt. Muktarun Islam Prity, mjini Sylhet, Bangladesh. Rifah amejiunga na Watu Mazingira Vijana.**



**Bi. Sally Titoyia Sengeny anafanya kazi na shirika la Africa Nature Organization n ani mmoja wa Mara-WE-Team, ambao wamepewa jukumu la kukuza biashara za wanawake eneo la Maasai Mara.**



**Mama Noonkuta Enole Dorop, P4N-462, Kaunti ya Narok ni mwanachama wa kwanza kusajiliwa kwa kikundi cha Wana-Biashara Wanawake cha Oloinyototo, eneo la Maasai Mara.**

**Mama Noonkuta alikuwa kiungo muhimu katika juhudi za kunda kikundi cha Oloinyototo na kwa kuruhusu kikundi kutumia ekari moja ya shamba lake kwa biashara endelevu za kimazingira.**

**Kupitia juhudi zake na viongozi wengine, waliweza kuandikisha wanachama 80 katika robo ya nne ya 2019.**

## Majukwaa

### Jukwaa La Maji

Mshirikishi: Silvanus Uunona (Namibia),

Mshirikishi Mwenza: Soledad Castro (Costa Rica).

### Jukwaa la Wanyama Pori na Misitu

Mshirikishi: Nancy Saumu Ronald (Kenya),

Mshirikishi Mwenza: Dorothy Syallow (Kenya).

### Jukwaa la Kilimo Hifadhi na Uvuvi

Mshirikishi: Yaa Tiwah (Ghana),

Mshirikishi Mwenza: Setondji Gaston (Gabon).

### Jukwaa la Elimi Hifadhi na Hamasa

Mshirikishi: Phathisani Tabengwa (Zimbabwe),

Mshirikishi Mwenza: Zelalem Abera (Ethiopia).

### Jukwaa la Vijana

Mshirikishi: Cheli Gurung (Nepal),

Mshirikishi Mwenza: Raymond Mwambire (Kenya).

### Jukwaa la Jamii Asili

Mshirikishi: Moses Ziro (Kenya),

Mshirikishi Mwenza: Jazzy Razalajaona (Malagasi).

### Jukwaa la Wanawake

Mshirikishi: Emma Kyomukama (Uganda),
Mshirikishi Mwenza: Ashengai Kimath (Tanzania).

### Jukwaa la Biashara Mazingira

Mshirikishi: Frank Maro (Tanzania),
Mshirikishi Mwenza: Fadhila Ghikas (Kenya).

## Kamati Kuu

1. Silvanus Uunona – Mwenyekiti,
2. Yaa Tiwaah – Mwenyekiti Mwenza,
3. Moses Ziro – Katibu Mkuu,
4. Frank Maro – Mweka Hazina,
5. Phathisani Tabengwa – Mwanachama,
6. Cheli Gurung – Mwanachama,
7. Nancy Saumu Pite – Mwanachama,
8. Emma Kyomukama – Mwanachama.

## Jarida la Watu Mazingira

1. Phathisani Tabengwa - Mhariri,
2. Catherine Musili - Mhariri Mwenza.

## Anuani

Vescon Estate 1, House No. 199, Felix Bunche Street, Bamburi, MOMBASA-KENYA.

## Anuani ya Posta

The People4Nature Global,

c/o Africa Nature Organization,

P.0 Box 2227-80100,

MOMBASA-KENYA.



People4Nature
Belong!

+254 780 127 800
+254 717 127 800

people4nature@africanature.or.ke

People4Nature Global